

# HALMASHAURI YA WILAYA YA LONGIDO

Barua zote ziandikwe  
kwa Mkurugenzi  
Mtendaji Wilaya. Simu  
No. 027-2539603/2 Fax:  
No. 027 – 2539603  
Tovuti:  
[www.longidodc.go.tz](http://www.longidodc.go.tz)



S.L.P 84,  
Longido

ARUSHA

## TANGAZO LA ZABUNI

02/05/2019


ZABUNI YA UWAKALA UKUSANYAJI WA MAPATO YA HALMASHAURI KWA VYANZO MBALIMBALI VYA MAPATO KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA LONGIDO KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020.

- Halmashauri ya Wilaya ya Longido imetathimini na kuainisha maeneo yenye shughuli za kiuchumi ikiwa ni pamoja na biashara, uzalishaji mali na uchimbaji wa maliasili za ardhini katika Wilaya kwa kipindi cha mwaka 2019/2020, Halmashauri imebaini kuwa ili kuleta tija, ufanisi na uwazi katika ukusanyaji wa mapato husika imedhamiria kuingia mikataba na mawakala mbalimbali wanaotambulika na kuidhinishwa kisheria na taasisi za serikali za ukusanyaji wa mapato (TRA).
- Halmashauri ya Wilaya ya Longido inakaribisha maombi kutoka kwa watu binafsi, vikundi mbalimbali na makampuni halali yenye uwezo na kukidhi masharti yalioainishwa kwenye nyaraka za zabuni husika,  
Orodha ya zabuni hizo ni kama ifuatavyo:

NAMBA YA ZABUNI	ENEO LA UKUSANYAJI
ZABUNI A; USHURU WA SOKO NA MNADA WA MIFUGO	
LGA/006/HQ/2019/2020/WAK/MIF/NCS/A/01	NOONDOTO
	SINYA
LGA/006/HQ/2019/2020/WAK/MIF/NCS/A/02	
LGA/006/HQ/2019/2020/WAK/MIF/NCS/A/03	MEIRUGOI
LGA/006/HQ/2019/2020/WAK/MIF/NCS/A/04	ENGARENAIBOR
LGA/006/HQ/2019/2020/WAK/MIF/NCS/A/05	NGEREYANI
ZABUNI NA D; USHURU WA GETI LA UTALII OLDONYO LENGAI	
LGA/006/HQ/2019/2020/WAK/GAT/NCS/B/01	LAKE NATRON
ZABUNI NA.F; USHURU WA MCHANGA, MAWE, MORAM NA KOKOTO	
LGA/006/HQ/2019/2020/WAK/MCH/NCS/C/01	OLTEPESI

- Waombaji halali na wenye nia wanatakiwa kuwasilisha taarifa zao binafsi ama za vikundi au makampuni, wakielezea maeneo yao ya upendeleo ikijumuisha uhai wa kikundi ama kampuni (company profile, certificate of incorporation, memorandum/articles of association), leseni ya biashara, usajili wa ulipaji kodi (VAT) na TIN.
- Waombaji waonyeshe uwezo wao wa kifedha kwa kuambatanisha hati za benki (bank statement) ikionyesha akiba isiopungua asilimia kumi na tano (15%) ya thamani ya mkataba wakala atakaosaini na Halmashauri kwa mwaka.
- Mzabuni awe na uwezo wa kujiwekea dhamana ya benki (Bank performance Security) ya asilimia kumi na tano (15%) ya mkataba wake wa mwaka mzima ambao atatakiwa kuiwasilisha katika Halmashauri ya Wilaya kabla ya mkataba kusainiwa.
- Mkataba utakaofungwa ni wa malipo ya kila mwezi.

7. Ada ya nyaraka ya zabuni ambayo haitarejeshwa hata kama mwombaji atakosa zabuni ya Tsh,100,000=(Laki moja) Italipwa kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Longido katika idara ya Fedha na kutolewa stakabadhi ya kupokelewa fedha na ambayo nakala yake itaambatanishwa katika barua ya maombi.
8. Mwombaji anaruhusiwa kuomba idadi yoyote ya uwakala isipokuwa kila eneo litakaloombwa litalipiwa, litafanyiwatathimini na kupewa mkataba wa kujitegemea.
9. Nyaraka ya zabuni ambayo mzabuni atajaza ipasavyo zinapatikana katika ofisi ya Katibu Bodi ya Zabuni iliopo kwenye jengo la ofisi kuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Longido chumba Na .32 kuanzia tarehe 02 /05/2019 muda wa kazi juma tatu hadi ijumaa kuanzia saa 2.00 asubuhi hadi saa 9.30 mchana.
10. Kwa ufafanuzi zaidi kuhusiana na zabuni hizi mawasiliano yafanywe kwa maandishi kupitia kwa Katibu wa Bodi ya Zabuni ya Halmashauri,S.L.P 84,Longido.
- 11.Mwombaji atatakiwa kujaza fomu iliopo kwenye nyaraka ya zabuni baada ya kufanya tathimini ya mapato na kuonyesha kiasi ambacho atalipa / atakachowasilisha kwenye Halmashauri kwa muda husika.
12. Makusanyo yote yatakusanywa kwa kutumia mashine za POS ambapo wakala atakayeshinda zabuni atakabidhiwa mashine hizo.
- 13.Maombi ya zabuni yaliyotayari yafungwe kwenye bahasha mbili,moja ya nakala halisi (original) na nakala mbili zilizorudifiwa zote zifungwe kwenye bahasha moja kwa lakiri na kuandikwa jina la uwakala ulioomba kama 'ombi la uwakala wa zabuni na;LGA/006/HQ/2019/2020/WAK/....JINA LA ZABUNI UNAYOOMBA” na kutumwa kwa katibu wa bodi ya zabuni ya Halmashari ya Wilaya ya Longido.S.L.P 84 Longido, chumba namba 32 kabla ya saa 05;00 asubuhi tarehe 23/05/2019.
14. Muda wa mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 23/05/2019 saa 5.00 asubuhi. Zabuni yeyote baada ya muda huo haitapokelewa.Ufunguzi wa zabuni utafuatia mara, waombaji au wawakilishi wao wanakaribishwa kuhudhuria sherehe za ufunguzi katika ukumbi mkubwa wa Halmashauri uliopo kwenye jengo la ofisi kuu ya Halmashauri.



(JUMAA M MHINA)

MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
HALMASHAURI YA WILAYA YA LONGIDO .

